# KWAHERI MPENDWA

Mazishi

Na. Faustine M. Majula
LUCHILI SUB-PARISH
28/08/2021.




2. Umeacha ndugu, jamaa na rafiki// wakikumbu-ka, mlivyoishi. (kumbuka mlivyoishi)
Nao kwa uchungu, tazama wanalia// machozi ya uchungu, yanawatika. (machozi yawatoka)

3. Umeacha mali, ulizo- tafuta// kweli hii dunia , ni- mapito. (dunia ni mapito)
Kwa juhudi kubwa, leo umeziacha// mali tulizonazo, nizakupita. (zote ni za kupita)

4. Ndu-gu safari, imeti-mia// hapa duniani, si kwako tena. (leo si kwako- tena)
Leo vazi lako, ni sanda jeupe// warudi mavumbini, tulikotoka. (vumbini tulikotoka)

5. Sote udongoni, tu-ta-ru-di// twa-ku-ombea, nenda salama. (twaomba nenda salama)
Umetangulia, nasitwa-fuata// ndugu ye-tu mpendwa, fika salama. (mpendwa fika salama)

6. Hi-lo jeneza, ndi-cho kitanda// na huo- udongo-, ndi-lo paa. (udongo ndilo paa)
hi-lo kaburi, ndiyo ya-ko nyumba// japo ni mzito, wakukandamiza. (unakukandamiza)

7. Mungu Baba Mwenyezi, a-ku-pokee// ukaishi kwake, milele yote. (uishi milele yote)
Kwe-nye makao, makao ya milele// nasi tutakapokuja, utupokee. (tujapo utupokee)

8. Hii ndiyo safari, sote tulongojea// twakuomba Baba, utupokee. (twaomba utupokee)
Tulitoka kwa Baba, kwake tutarejea// turudipo kwako, tuishi milele. (tukaishi milele)

N.B:- Badala ya neno Mpendwa waweza tumia jina halisi.
- Maneno yaliyo kwenye mabano yaimbwe na sauti ya III na IV kwa kufuata nota zao zilivyo kwenye Muziki.
- Zingatia matumizi ya alama (, na //) kama zilivyotumika kwenye Muziki.

majulafaustine99@gmail.com